JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA FEDHA**

# MAELEZO YA MHESHIMIWA BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (Mb), WAZIRI WA FEDHA AKIWASILISHA KATIKA KAMATI YA BUNGE ZIMA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2026/27

**11 MACHI, 2026**

**MAELEZO YA MHESHIMIWA BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (Mb), WAZIRI WA FEDHA AKIWASILISHA KATIKA KAMATI YA BUNGE ZIMA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2026/27**

## 1. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana siku hii ya leo kwa ajili ya kuw Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ninawasilisha Mapendekezo ya Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27 kwa mujibu wa Ibara ya 137(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 23 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Kanuni ya 119 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la Mwaka 2025. Mapendekezo ninayowasilisha yamegawanyika katika sehemu kuu nne: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26; Sehemu ya Tatu ni Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/27; na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

## 2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2025/26

3. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika bajeti ya mwaka 2025/26, Serikali ililenga kufikia malengo na shabaha za uchumi na bajeti ambapo utekelezaji wake unaonesha kufikiwa kwa mafanikio mahsusi kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera, mikakati na mipango mbalimbali inayoendelea kutekelezwa na Serikali. Matokeo ya utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ya Serikali ni kama ifuatavyo:

(i) Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2025, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024;

(ii) Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Pamoja na ongezeko la wastani wa mfumuko wa

bei katika kipindi hicho, kiwango cha asilimia 3.5 kiko ndani ya lengo la nchi la asimilia 3 hadi 5; na

(iii) Hadi Desemba 2025, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 6,329. Kiasi hicho kilitosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.9 ikilinganishwa na lengo la miezi 4.0.

4. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali katika kipindi cha Julai – Desemba 2025 inaonesha mwenendo mzuri wa viashiria vya uchumi jumla, hivyo malengo ya mapato ya ndani na mapato ya kodi ya kufikia asilimia 16.7 na asilimia 13.3 ya Pato la Taifa mtawalia mwishoni mwa mwaka 2025/26 yanatarajiwa kufikiwa. Aidha, malengo ya naksi ya bajeti isiyozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa yanatarajiwa kufikiwa kama ilivyopangwa.

5. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2025/26 ni shilingi bilioni 56,490.3. Bajeti hii inagharamiwa na mapato ya ndani shilingi bilioni 40,466.1, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilingi bilioni 1,069.9, na nakisi ya bajeti inagharamiwa na mikopo ya ndani shilingi bilioni 6,278.2 na mikopo ya nje shilingi bilioni 8,676.1.

6. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, Serikali ilifanikiwa kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 28,215.4.

### 2.1. Mwenendo wa Mapato

7. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Hadi Desemba 2025, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 20,303.0, sawa na asilimia 99.1 ya lengo la nusu mwaka na yaligharamia asilimia 72.0 ya mahitaji ya kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 16,908.2, sawa na asilimia 103.0 ya lengo. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha uhiari wa kulipa kodi pamoja na kuongezeka kwa wigo wa vyanzo vya mapato ya kodi kufuatia kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, mifumo ya usimamizi wa vyanzo vya mapato na ufanisi katika usimamizi wa mikakati ya kiutawala. Mapato mengine (mapato yasiyo ya kodi) yalikuwa shilingi bilioni 3,394.8, sawa na asilimia 83.0 ya lengo la nusu mwaka. Misaada ilikuwa shilingi bilioni 507.6, sawa asilimia 95.7 ya lengo na asilimia 1.8 ya bajeti yote ya nusu mwaka.

### 2.2. Mwenendo wa Matumizi

8. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025,

matumizi bila malipo ya mitaji yalikuwa shilingi bilioni 25,060.0, sawa na asilimia 100.8 ya lengo la kipindi hicho. Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 7,404.9 kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa ajili ya kulipa mikopo iliyoiva (rollover) na kugharamia miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 103.9 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3,155.4 zilitumika kulipa mitaji iliyoiva (rollover) na shilingi bilioni 4,249.5 kugharamia nakisi ya bajeti, hususan utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

9. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mafanikio mbalimbali yamepatikana katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:

(i) Kulipa mishahara ya watumishi na kugharamia deni la Serikali kwa wakati ambapo jumla ya shilingi bilioni 9,704.3 zilitumika;

(ii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja wa asilimia 3.5 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025;

(iii) Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha asilimia 6.0 katika kipindi cha miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024;

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kielelezo ikiwemo ujenzi wa SGR ambapo shilingi bilioni 630.4 zilitumika hadi Novemba 2025, miradi ya kuzalisha na kusambaza umeme shilingi bilioni 158.8 na uendelezaji wa mji wa Serikali Mtumba shilingi bilioni 225.8;

(v) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya kodi na kuvuka lengo kwa asilimia 2.4 na ukuaji wa asilimia 19.1 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024/25;

(vi) Kuendelea kugharamia mahitaji ya sekta za huduma za jamii ikiwemo mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya kati na elimu ya juu, elimu bila ada kwa shule za msingi na sekondari, dawa, vifaa na vifaa tiba, pamoja na usambazaji wa maji safi na salama ambapo jumla ya shilingi bilioni 8,973.5 zimetolewa kwa ajili ya sekta za huduma za jamii;

(vii) Kufanikisha mashindano ya CHAN 2024 kwa kushirikiana na Kenya na Uganda ambayo yalifanyika Agosti 2025, ambapo Tanzania ilinufaika kwa kuongeza fursa za shughuli za kiuchumi, kijamii na ajira, kupanua wigo wa mahusiano ya kidiplomasia pamoja na kukuza shughuli za utalii. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya michuano ya AFCON 2027 ambapo shilingi bilioni 146.0 zimetolewa na kutumika; na

(viii) Kuendelea kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi wa umma, wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ambapo jumla ya shilingi bilioni 194.7 zimetumika na hivyo kuchachua shughuli za kiuchumi.

## 3. MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI KWA MWAKA 2026/27

### 3.1. Malengo na Misingi ya Uchumi Jumla

10. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2026/27 ni kama ifuatavyo:

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2026;
(ii) Mfumuko wa bei kuwa kwenye wigo wa tarakimu moja ya kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0;
(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27;
(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27;
(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na
(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

11. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mapendekezo ya mfumo na ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27 yameandaliwa kwa kuzingatia misingi ya uchumi jumla ambayo ni:

(i) Utekelezaji wa Mkakati wa Ukusanyaji Mapato wa Muda wa Kati (Medium Term Revenue Mobilization Strategy) 2025/26 – 2027/28;
(ii) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;
(iii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, tetemeko la ardhi, magonjwa ya mlipuko, mafuriko na migogoro ya kivita na kibiashara;
(iv) Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;
(v) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na
(vi) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

### 3.2. Sera za Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2026/27

12. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa mwaka wa fedha 2026/27, Serikali

itaendelea kutoa kipaumbele katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi. Mikakati ya kuongeza mapato ya ndani ni pamoja na: kurasimisha sekta isiyo rasmi; kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari; kuhamasisha na kusimamia matumizi sahihi ya mashine za risiti za kielektroniki (EFD); kuimarisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji mapato na matumizi; kuhimiza matumizi ya njia za malipo za kibenki na kielektroniki; kurasimisha na kumilikisha ardhi ili kupanua wigo wa mapato; pamoja na kuimarisha miundombinu, mifumo na vitendea kazi kwa ajili ya kuwezesha mafungu, taasisi na mashirika ya umma kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

13. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa upande wa matumizi, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 ili kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Aidha, Serikali itaweka mkazo katika upembuzi yakinifu kwa miradi yote, kusimamia miradi kwa weledi, kujiridhisha na kuheshimu matakwa ya mikataba inayoingiwa ili kudhibiti mianya ya mashtaka kwa Serikali na hivyo kuepuka gharama za kuvunja mikataba husika. Aidha, Serikali itajikita katika kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA; kukamilisha miradi inayoendelea; kuboresha usimamizi na utendaji wa taasisi na mashirika ya umma; na kufungamanisha miradi ya maendeleo inayofanana baina na miongoni mwa sekta.

14. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, utengaji wa fedha utazingatia mahitaji ya msingi yasiyoepukika ikiwemo mishahara na huduma za deni la Serikali, malimbikizo ya madai, madeni na ugharamiaji wa miradi ya kipaumbele inayofungua fursa za kiuchumi kama ilivyobainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 ikiwemo ujenzi wa miundombinu wezeshi ya kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi.

### 3.3. Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2026/27

15. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Mwaka 2026/27 yamezingatia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ulioainisha vipaumbele vikuu vitano (5) ambavyo ni utawala, amani, usalama na utulivu; kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani utakaotekelezwa kupitia sekta tisa (9) za mageuzi; kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; na vichocheo vya mageuzi. Aidha, Serikali itaweka msukumo katika:

kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; ulipaji wa mishahara na deni la Serikali; ukamilishaji wa miradi na programu za maendeleo zinazoendelea; na kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza katika miradi yenye tija itakayochochea ukuaji wa uchumi, kuongeza fursa za ajira na mapato kwa Serikali.

## 3.4. Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/27

16. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa kuzingatia sera za bajeti na mikakati ya kukusanya mapato pamoja na udhibiti wa matumizi, Serikali inakadiria kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 62,334.2 mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la asilimia 10.3 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/26. Ukomo huu umefikiwa baada ya kuzingatia vigezo kadhaa ikiwemo: mwenendo halisi wa mapato ya ndani; ukomo wa nakisi ya bajeti usiozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa; ongezeko la deni la Serikali, gharama za mikopo katika soko la fedha na ongezeko la malipo ya mikopo; mahitaji ya ajira mpya; na mabadiliko ya sera za washirika wa maendeleo.

### 3.4.1. Mapato

17. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mapato yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 46,791.3 ambapo mapato ya kodi ni shilingi bilioni 36,989.3, mapato mengine ni shilingi bilioni 9,238.8 (ikiwemo mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya shilingi bilioni 1,966.2) na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 563.1. Aidha, makadirio ya mapato ya ndani (kodi na mengine) ni sawa na asilimia 74.2 ya bajeti ya mwaka 2026/27. Kwa kuzingatia malengo ya Dira 2050, Serikali itaendelea kutumia njia mbadala za kugharamia miradi na kuandaa miradi inayokopesheka ili sekta binafsi itumie fursa hiyo kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

### 3.4.2. Matumizi

18. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, matumizi na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha bila kujumuisha malipo ya mtaji ni shilingi bilioni 54,498.6 ambapo kati ya kiasi hicho, stahiki za watumishi ikijumuisha michango ya pensheni ni shilingi bilioni 9,985.7, gharama za bidhaa na huduma shilingi bilioni 8,302.9, malipo ya riba shilingi bilioni 7,257.9, ruzuku shilingi bilioni 24,942.0 na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi bilioni 3,030.4.

19. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 15,542.9 kwa mwaka 2026/27. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya ndani ni shilingi bilioni 6,557.7, mikopo ya nje yenye masharti nafuu shilingi bilioni 6,554.8 na

mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 2,430.4. Aidha, mikopo halisi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 7,707.3 na malipo ya mtaji (rollover) ni shilingi bilioni 7,835.6.

20. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mchanganuo wa mapendekezo ya mfumo wa bajeti kwa mwaka 2026/27 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1**.

## Jedwali Na. 1: Mapendekezo ya Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27

(shilingi milioni)

| | 2025/26 | | 2026/27 | |
|---|---|---|---|---|
| | Bajeti Iliyoidhinishwa | Bajeti iliyoboreshwa | 2026/27 Bajeti Inayopendekezwa | Ongezezo |
| **A: Mapato** | **41,536,016** | **41,391,220** | **46,791,299** | **13.0%** |
| Mapato ya kodi | 32,306,123 | 32,306,123 | 36,989,320 | **14.5%** |
| Misaada/Michango | 1,069,884 | 925,088 | 563,139 | **-39.1%** |
| Mapato mengine | 8,160,009 | 8,160,009 | 9,238,839 | **13.2%** |
| o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,680,507 | 1,680,507 | 1,966,193 | **17.0%** |
| | | | | |
| **B: Matumizi** | **45,994,829** | **45,994,829** | **51,468,233** | **11.9%** |
| **Mishahara na stahiki za watumishi** | **7,711,867** | **7,711,867** | **9,985,742** | **29.5%** |
| o/w Mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu | 4,754,850 | 4,754,850 | 5,324,212 | **12.0%** |
| Michango ya hifadhi za jamii | 2,240,141 | 2,240,141 | 2,569,421 | **14.7%** |
| **Gharama za bidhaa na huduma** | **7,812,245** | **7,812,245** | **8,302,857** | **6.3%** |
| o/w Malipo ya madeni ya watumishi, wazabuni na wakandara | 700,000 | 700,000 | 800,000 | **14.3%** |
| **Malipo ya riba** | **6,493,715** | **6,493,715** | **7,257,876** | **11.8%** |
| Malipo ya riba nje | 2,796,427 | 2,796,427 | 3,000,302 | **7.3%** |
| Malipo ya riba ndani kwa taasisi zisizo Serikali Kuu | 3,697,288 | 3,697,288 | 4,257,574 | **15.2%** |
| Malipo kwa taasisi ambazo ni Serikali Kuu | - | - | | |
| **Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji** | **1,936,023** | **1,936,023** | **2,032,825** | **5.0%** |
| Kwa mashirikia ya umma | 1,889,293 | 1,889,293 | 1,983,758 | **5.0%** |
| Kwa sekta nyingine | 46,730 | 46,730 | 49,067 | **5.0%** |
| **Ruzuku na michango** | **21,107,935** | **21,107,935** | **22,909,238** | **8.5%** |
| Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa | 9,703,349 | 9,703,349 | 10,412,288 | **7.3%** |
| o/w Mishahara ya watumishi | 6,162,616 | 6,162,616 | 6,470,747 | **5.0%** |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 1,793,891 | 1,793,891 | 1,883,585 | **5.0%** |
| Kwa taasisi za umma | 11,404,586 | 11,404,586 | 12,496,950 | **9.6%** |
| o/w Mishahara ya watumishi | 2,183,984 | 2,183,984 | 2,293,183 | **5.0%** |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 6,819,691 | 6,819,691 | 7,160,676 | **5.0%** |
| **Mafao na misaada ya kijamii** | **752,516** | **752,516** | **790,141** | **5.0%** |
| Mafao ya hifadhi za jamii | - | - | | |
| Misaada ya huduma za jamii | 10,473 | 10,473 | 10,997 | **5.0%** |
| Mafao na viinua mgongo | 742,042 | 742,042 | 779,144 | **5.0%** |
| **Gharama nyingine** | **180,528** | **180,528** | **189,554** | **5.0%** |
| | | | | |
| **Salio la Mapato na Matumizi** | **(4,458,813)** | **(4,603,609)** | **(4,676,935)** | **1.6%** |
| | | | | |
| **C: Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha** | **2,780,160** | **2,780,160** | **3,030,375** | **9.0%** |
| Gharama za majengo, miundombinu, mashine n.k | 2,666,037 | 2,666,037 | 2,905,980 | **9.0%** |
| Mali zisizozalishwa/mali za asili | 114,123 | 114,123 | 124,394 | **9.0%** |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti bila Misaada** | **(8,308,858)** | **(8,308,858)** | **(8,270,449)** | **-0.5%** |
| | | | | |
| **Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada** | **(7,238,973)** | **(7,383,770)** | **(7,707,309)** | **4.4%** |
| | | | | |
| **Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti** | 7,238,973 | 7,383,770 | 7,707,309 | **4.4%** |
| **Mikopo halisi** | **7,238,973** | **7,383,770** | **7,707,309** | **4.4%** |
| **D: Mikopo ya ndani** | **2,952,630** | **2,214,112** | **3,272,349** | **47.8%** |
| D1 - Mikopo ya ndani | 6,278,186 | 5,539,668 | 6,557,744 | **18.4%** |
| D2 - Malipo ya mikopo ya ndani | (3,325,557) | (3,325,557) | (3,285,395) | **-1.2%** |
| | | | | |
| **E: Mikopo ya nje** | **4,286,343** | **5,169,658** | **4,434,960** | **-14.2%** |
| E1 - Mikopo ya nje | 8,676,050 | 9,559,364 | 8,985,150 | **-6.0%** |
| o/w Mikopo ya Kibiashara | 2,629,012 | 2,629,012 | 2,430,372 | **-7.6%** |
| E2 - Malipo ya mikopo ya nje | (4,389,707) | (4,389,707) | (4,550,190) | **3.7%** |
| | | | | |
| **Jumla ya Bajeti ( A + D1 + E1)** | **56,490,252** | **56,490,252** | **62,334,193** | **10.3%** |
| **Nakisi ya bajeti/Pato la Taifa** | **-3.0%** | **-3.0%** | **-2.9%** | |

**Memo Items**


| | | | |
|---|---|---|---|
| Pato la Taifa | 42,071,490 | 244,548,703 | 269,855,032 |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## 4. HITIMISHO

21. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa mwaka 2026/27, Serikali inatarajia kuendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo Mkakati wa Muda wa Kati wa Kuongeza Mapato 2025/26 – 2027/28 ili kuongeza wigo wa kodi na hivyo kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kupunguza utegemezi wa kibajeti. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia na kudhibiti matumizi yasiyo na tija, kuwianisha mahitaji na hali halisi ya upatikanaji wa mapato, na kutoa kipaumbele kwa mahitaji yasiyoepukika ikiwemo ugharamiaji wa mishahara, deni la Serikali, hati za madai na huduma za jamii. Vilevile, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele kama ilivyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 na kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea.

22. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** naomba kuwasilisha.



**Mh. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb),**
**WAZIRI WA FEDHA**
**Machi 10, 2026**